TEMEKE MUNICIPAL COUNCIL.
MIKWAMBE SECONDARY SCHOOL.
P.O Box 36014 Dar es salaam, 0625 522 980 & 0787 615 977 E-mail: mikwambesekondarischool@gmail.com

MZAZI/MLEZI WA …….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI

1.0 Utangulizi

Ninakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Mikwambe mwaka 2021. Shule ya Sekondari Mikwmbe ipo Manispaa ya Temeke, Kata ya Toangoma katika Mtaa wa Mikwambe–CCM. Usafiri wa daladala unapatikana katika vituo vya Toangoma (Stend Mpya) na Kigamboni.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza Tarehe 11/01/2021, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni katika kipindi cha siku tano (5) kuanzia tarehe 06/01/2021.

Siku ya kuripoti shuleni ni lazima mwanafunzi aambatane na mzazi au mlezi anayemsimamia.

2.0 Mambo Muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya Shule

a. Wavulana
- Suruali mbili (2) nyeusi zisizo na pindo, zisiwe modal).
- Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi (pamba) zenye alama ya kuonesha kidato.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba(visiwe buti, sendo wala visiwe na visigino virefu).
- Soksi nyeusi jozi mbili(2).
- Tai mbili(2)nyeusi.
- T-sheti ya shule (Huvaliwa siku za Jumatano na Ijumaa).

b. Wasichana
- Sketi mbili (2) ndefu nyeusi (mshono-rinda box zisiwe na mkanda)
- Shati mbili nyeupe za mikono mifupi au nusu kanzu nyeupe na hijab nyeupe(pamba) zenye nembo ya shule.
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba (visiwe buti, sendo wala visiwe na visigino virefu),
- Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- Tai mbili (2) nyeusi (kwa wanaotumia shati),
- T-sheti ya shule (Huvaliwa siku za Jumatano na Ijumaa)

2.2 Vifaaa vya kujifunzia

- Daftari kubwa (counter book) angalau kumi (10).
- Kalamu za wino.
- Mkebe wa hisabati.
- Dictionary (kamusi)
- Graph pad.
- Mkoba wa kubebea vifaa (begi).
- Vitabu vya masomo mbali mbali.

2.3 Kitambulisho cha shule

2.4 Nauli ya kuja na kurudi toka shule pamoja na hela ya kutosha ya matumizi binafsi ya chakula awapo shuleni.

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yen ye dhamana ya Elimu Tanzania na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji ya elimu.

Unatakiwa kuzingitia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utakabidhiwa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule kwa usahihi wakati wote unaotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali ya umma.

3.1 Makosa Yanayoweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
e) Kupigana au Kupiga
f) Kuharibu kwa makusugi mali ya umma
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito.
i) Kuoa au kuolewa

j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu
m) Kuwa na simu ya mkononi

3.2 Makosa Yanayoweza Kusababisha Kusimamishwa Masomo.

a) Kuvaa pete
b) Kunyoa nyusi
c) Kuvaa hereni
d) Kupaka hina kwenye kucha au sehemu nyingine za mwili
e) Kuwa na kucha ndefu
f) Kuwa na nywele ndefu, kusuka, kukali au kurilax
g) Kunyoa kipara au Mitindo
h) Uvaaji usioridhisha wa sare ya shule (sketi fupi, suruali ya kubana mwili, mlegezo) na kuvaa nguo zisizokubalika uwapo shuleni
i) Kufuga ndevu

4.0 Mambo Mengine Muhimu Yanayopaswa Kakamilishwa na Kuwasilishwa Shuleni na mwanafunzi

a. Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospital ya Serikali. Fomu itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapowasili shuleni.
b. Fomu ya maelekezo binafsi ya mwanafunzi na wazazi/walezi wake, kuhusu historia yake.
c. Fomu ya mwanafunzi na mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria kanununi na maelezo mengine yatakayotolewa na shule (mkataba wa kutokushiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.)

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

HATIBU O. JONGO

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE

SHULE YA SEKONDARI MIKWAMBE

FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

Jina la mwanafunzi ……

Tarehe ya kuzaliwa ……

PICHA YA MWANAFUNZI

0787 615 977 (Mkuu wa Shule) 0717 434 816/0756969 542 (Makamu Mkuu wa Shule)

Uraia ……..

Mahali alipozaliwa (Mkoa na Wilaya) ……..

Dini …….

Shule aliyohitimu darasa la saba ……

Mtaa unaoishi …….

Jina la mjumbe wa mtaa……. Simu ……..

TAARIFA YA WAZAZI/WALEZI

a. Mzazi/Mlezi wa kwanza
Jina la mzazi/mlezi …….
Uraia …….. Kazi ……..…..
Uhusiano na mwanafunzi……
Sehemu anayoishi ……..
Namba ya simu ……...
Kazi …….…….. Simu (anapofanyia kazi)…….
Jina la mjumbe wa mtaa …… Simu ……..

PICHA YA MZAZI

b. Mzazi/Mlezi wa pili
Jina la mzazi mlezi ……..……
Uraia ……. Kazi …….……
Uhusiano na mwanafunzi ……...…….
Sehemu anayoishi ……..
Namba ya simu ……...
Kazi …….. Simu (anapofanyia kazi)……..…….
Jina la mjumbe wa mtaa …… Simu ……

PICHA YA MZAZI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
SHULE YA SEKONDARI MIKWAMBE

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

A. MWANAFUNZI
Mimi ……. (jina kamili), ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha …… Mwaka …… katika shule ya Sekondari Mikwambe.

NINAAHIDI KWAMBA
i. Nitazingatia na kutii sheria zote za shule
ii. Nitafanya bidii katika masomo na shughuli zote za shule
iii. Nitashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali

iv. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hatanikiwa nje ya shule kwa dhumuni la kuipa na kutunza sifa ya shule
v. Kwa namna yoyote sitashiriki katika fujo au migomo yoyote

Sahihi ……. Tarehe ……

B. KWA MZAZI/MLEZI

Mimi……(jina kamili)

Ninaahidi kwamba_;

i. Nitashiriki kikamilifu katika kusimamia maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma na kinidhamu
ii. Nitampatia mwanafunzi mahitaji yote ya shule yaliyoainishwa katika fomu ya kujiunga na shule na mengine yatakayojitokeza
iii. Nitakuwa tayari kutoa usaidizi wowote utakaohitajika katika kumlea mwanafunzi
iv. Nitakagua na kumhimiza mwanafunzi kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani na kufuatilia maendeleo yake shuleni.
v. Mwanafunzi awapo nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake
vi. Nitaitikia wito na kushiriki vikao vyote vya wazazi kila mara nitakapohitajika.

Sahihi ya mzazi/mlezi…….....tarehe…….

TEMEKE MUNICIPAL COUNCIL

MIKWAMBE SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

To be filled by the government medical officer and return to the Head of School

STATION ……..

DATE ……

STUDENT'S NAME: ……

Please examine the above named as to her/his fitness for admission as a student in the following common diseases/problems:-

Put tick (v) whenever student found positive or negative in a list of the following disease.

S/No	TEST	POSITIVE	NEGATIVE
1	Pregnancy (for Female)		
2	Asthma		
3	Diabetes		
4	Worms		
5	Epilepsy		
6	TB (tuberculosis)		
7	Sickle Cell		
8	Heart Disease		
9	Yellow Fever		
10	U.T.I		
11	Malaria		

I have examine the above named and consider that she/he is physical fit/unfit for admission

Designation…….. Signature …….. Date …….